# NI LAZIMA SWALA LA MAOMBI LIPEWE KIPAUMBELE NA KILA MTEULE KATIKA MAISHA YAKE YA KILA SIKU

## Maandiko: MARK. 1: 35, DAN. 6: 10

## 1. UTANGULIZI:

Kufanya maamuzi au wakati mwingine mteule kuwa na maandalizi ya mambo Fulani siyo vibaya kama ilivyo katika ***mithali 16:1,*** lakini maamuzi yoyote yale au maandalizi yoyote yale kama **hayataatamiwa** na maombi ni sawa na kuku anayetaga mayai lakini akakosa muda wa kuyaatamia; kamwe asitarajie kupata vifaranga (kuangua vifaranga)

- Ndiyo sababu nataka niwausie wanangu leo kuwa maamuzi yako ya kuishi maisha matakatifu hapa duniani na kutomtenda Mungu dhambi lazima **yashikiliwe** na maombi!!! ***Dan. 6:10*** – Maombi ya kuugua, yaliyojaa maumivu na uchungu wa kuhitaji msaada kutoka kwa Mungu ndiyo daima yanayoleta suluhisho katika dhoruba nyingi tunazokutana nazo katika maisha haya; **lakini zaidi sana nimegunduwa ya kwamba maombi ya kina/ya kujimimina ndiyo yanayounidhamisha huu huu mwili!!!** Kuamua jambo halafu ukakosa kuliombea ni kujidanganya kama tutakavyoona huko mbele, ndiyo sababu Daniel alipoamua kutojitia unajisi ***(Dan. 1:8),*** aliamua kuwa mwombaji na maamuzi yake haya yakashikiliwa na maombi na hatimaye akawa mshindi.

2. Yesu wakati anahitimisha hotuba yake ya mlimani alisema maneno mazito mno “ ***Math. 7:24-29.*** Ni muhimu sana kila mwanafunzi kuelewa jambo hili kwamba ushindi wa leo siyo ushindi wa kesho; na mvua aliyoisema hapa Yesu pamoja na mafuriko aliyoyataja hapa na kisha pepo zilizovuma alikuwa anamaanisha majaribu ya aina mbalimbali **yatakovurumishwa** na ibilisi katika maisha yetu tulioamini kama **yalivyovurumishwa** kwa Danieli na mwenzake, **bila mteule kuwa na maandalizi na mipango madhubuti ya maombi kila siku; Kesho watu watasimulia historia nyingine ya mteule**

**huyo kabisa.** Yesu anasema **" wote tutapigwa na mafuriko, lakini kitakachotutofautisha ni maandalizi ya kila mmoja**

- **Mojawapo ya sifa kuu aliyonayo ibilisi ni kutokata tamaa!!** ukimpiga na kumshinda leo, kesho anakuja na stahili nyingine ulivyomshinda mwaka jana, mwaka huu atakuja na mtindo mwingine **1Wafalme. 20:21–22**, na lengo lake kubwa ni kupepeta Kanisa (kulitawanya) ili lisiwepo kabisa, lakini kwa maombi ya kina anashindwa kila siku**. *Luk. 22: 24 - 34.* Jaribu linalomshinda mtu na kupelekea kuiacha imani; jaribu lile lile kwa mtu mwombaji anavuka salama na kwa ushindi mkubwa**.

  **Note:** Petro ndugu zangu hakuwa mtu mdogo kamwe; yeye alishatembea hata juu ya maji (ana imani), yeye alikuwa ni Mtume wa kufanya maamuzi magumu; alishamwona Yesu katika utukufu wake; ameshuhudia kwa macho yake ya nyama Yesu akifufua wafu, **Math.14: 27- 29, Math. 17:9, Mark.5:35 - 43** Alipata uzoefu hapa Petro. **Mdo. 9: 39-42)** Pamoja na yote haya, alipoacha kuomba, alifanya kituko cha ajabu na akamkana Yesu kabisa. **Math. 26:36-54, Yoh. 18:1-27.**

- Au nabii Eliya ndugu zangu siyo nabii mdogo hata kidogo, alishafunga mvua na haikunyesha kwa miaka $3^{1/2}$ hadi alipoifungua tena; alishaishi kwa kuhudumiwa na kunguru; alishafufua mfu, alishashusha moto wa ajabu uliokuwa unalamba maji, alishaua manabii wa Baali **450** n.k. bado shetani hakukata tamaa, na alipolegea na kukosa maombi na waombezi Eliya alijiombea afe na kujihukumu kwamba yeye siyo mwema kuliko Baba zake!!
  ***1Wafal .19:1-21***

- **Kuishi ndani ya wokovu bila ya kuwa na maombi binafsi ya kina kila siku alfajiri, unaishi kwa hatihati (probability**) unakuwa na sura mbili!! **lakini watu imara na wasiotikiswa na mvua za mafuriko na pepo zinazovuma juu yao kama Daniel (consistence/stable people), watu walio na msimamo usiyoyumba; daima maombi yalikuwa ndiyo silaha yao muhimu sana. Maombi ni kama kinoo kinachorudisha makali**

**kwenye visu (mapanga/shoka baada ya kuwa vimetumika na makali kukamalizika.**

**Note : kufanya maamuzi ya kujitofautisha na ulimwengu huu ni jambo moja muhimu sana kama Daniel alivyoazimia kabisa tangu mwanzo *(Dan.1:8*) lakini maombi yake ya mara kwa mara ndiyo yaliyonidhamisha mwili wake wakati wote hata asiogope kufa wakati wowote.**

- Mtu mwombaji wa maombi ya kuzama daima ndiye anayemchanganya daima shetani katika uwanja wa mapambano hadi anakosa maeneo ya kushikilia kama mashitaka kwa Mungu wetu aliye hai ***Dan. 6:4-28 (Dan. 6:4)*** Ni lazima tufike mahala pa shetani kutuheshimu na kupiga nahesabu kwamba huyu ni mwiingieje na siyo kutuangusha tu hovyo hovyo kwa vitu vya hovyo hovyo!! Anaweza akavumisha tu leo imani Fulani potofu, au akavumisha magonjwa tu kama haya ya Corona, au jaribu Fulani tu la watoto, au akavumisha tu mafanikio usiyoyatarajia au akayumbisha tu uchumi wako n.k. mtu aliye na maamuzi thabiti ya kumpendeza Yesu kwa gharama zozote na ambaye anadumu katika maombi; badala ya pepo hizi zilizovumishwa na shetani kumkatisha tamaa, yeye ndiyo anaimarika zaidi. ***Ayub 1:8-22*** na ***Filp. 4:10-13***. Bila kuwa mwombaji wa kuzama katika nyakati hizi, tutatupwa huku na kule na Wakristo wa uongo na manabii wa uongo. ***Efes 4:14***

**Note.katika Biblia kuna watu waliofanya mambo ya kushangaza sana, lakini wakamaliza safari yao vibaya sana – mfano- Samsoni yeye katika maisha yake aliomba mara mbili!! tena aliomba wakati alipokuwa anakabiliana na dhiki; siku nyingine zote za maisha yake alikwenda kwa uzoefu!!**
***Waam. 15:17-20, 16: 23-31.***
Ndivyo ilivyo hata katika siku zetu, mtu yeyote anayeacha maombi na kuishi ndani ya wokovu kwa mazoea tu atafanya vituko vya kushangaza wengi hata kama hukonyuma alikuwa ameshuhudia mengi kama Petro katika maisha yake ya wokovu

3. **Ndiyo sababu Yesu aliyapa maombi kipambaumbele no 1 kama tulivyoona katika *Mark. 1:35.* Yeye alijali sana kuwa na faragha na Baba yake kwanza ndipo mambo mengine yafuate. Ratiba yake ya maombi hakuruhusu iingiliwe na jambo lingine lolote hasa maombi ya Alfajiri na mapema. Maombi ya Alfajiri kwa Yesu ndiyo yalikuwa yanampa dira (uongozi) sahihi wa jinsi atakavyotumika kwa siku nzima.** Ni vyema basi kuanzia leo kila mteule akatenga muda wa alfajiri na mapema kuwa muda wake wa kukuza mahusiano yake binafsi na Mungu Baba; Mwana wa Roho Mtakatifu kwa njia ya kuzungumza nae ( kuomba) ili kupata uongozi/dira ya siku nzima utumikaje

- Alfajiri ni muda mzuri sana wa kujenga mahusiano yetu na Mungu Baba, Mwana pamoja na Roho Mtakatifu kwa sababu unapata muda wa kutosha wa kukaa na kuzungumza naye vya kutosha kwa njia ya maombi
- Kumbuka daima kwamba unapokuwa na muda binafsi na Mungu tabia zako za kiungu **zinakuzwa** ndani yako na Mungu Roho Mtakatifu mwenyewe

**Note.** Kuna mambo matatu makubwa ya kiroho ambayo shetani anapambana nayo usiku na mchana kwa wateule na **mojawapo ni eneo la Maombi. Hataki kabisa tuombe maana anafahamu fika kwamba silaha ya maombi ni silaha ya maangamizi kwake na ni silaha ya ushindi kwa wateule‼ *2 Nyak 20:1-30* 23 Mdo. 12:5-9* 18-19. Maombi yanamchanganya kabisa ibilisi katika uwanja wa mapambano. Maombi yanavuruga mipango yake kabisa. *2Wafal 6:8-14, 18-23***

- Hebu kila mteule kuanzia sasa alipe eneo la maombi na hasa maombi ya alfariji, maombi ya binafsi kipambaumbele cha kwanza na kwa muda mfupi ataona mabadiliko yasiyo ya kawaida katika maisha yake, na adui atachanganyikiwa muda siyo mrefu na ushindi wa kishindo utadhihirika katika maisha yako daima.

**Na**
**Askofu Dr. L. M. Mwizarubi**
**Oct 2021**